REGISTRY COPY

HAKIARDHI

# ARDHI NI UHAI

ISSN NO. 0856-9495 TOLEO LA 05 Mei - Agosti 2007


# KUMBUKIZI YA PROFESA CHACHAGE S.L CHACHAGE

## CHACHAGE YU KATI YETU JAPO HAONEKANI

*Na Yefred Myenzi*

Hakuna kazi ngumu kama ya kutoa wasifu wa mtu ambaye ametumia muda mwingi wa maisha yake katika harakati mbalimbali za mapambano ya kifkra na kijamii katika ngazi tofauti. Inakuwa kazi ngumu kwasababu kila ukifanya jitihada ya kuandika moja unahisi na wakati fulani unatambua kuwa umesahau au umeacha jingine la muhimu zaidi ama hujafanya inavyotakiwa. Naamini hali hii haitanikumba mimi pake yangu bali pia wenzangu wengi ambao watajaribu kufanya kumbukizi ya namna yoyote ya marehemu Profesa Chachage mwanazuoni mahiri aliyetutoka ghafla na kutuachia simanzi isiyoisha mwaka mmoja uliopita. Haikuwa rahisi kuamini kuwa Profesa Seith Lothi Chachage hatutakuwa naye tena kwa watu wengi waliopata taarifa hizi ile Julai tisa na ndivyo isivyo rahisi kumwelezea wasifu wake leo hii baada ya mwaka mmoja kwa kurasa chache za karatasi za kawaida kama hizi ukaridhika kuwa umemtendea haki.

Hata hivyo, itosheleze tu kusema kuwa Chachage msomi wa kiafrika, muumini wa falsafa za ukombozi, uhuru, Endelea Uk.3



Profesa Chachage enzi ya Uhai wake akiwa kwenye chumba cha majadiliano kuhusu Asasi za Kiraia yaliyoandaliwa na HAKIARDHI mjini Morogoro mwezi Februari 2006.

### NUKUU YA LEO

*"Lau kungekuwa na aina yeyote ile ya kuwezesha baadhi ya watu wema wenye busara na hekima wasipatwe na mauti, basi jamii ingekuwa tayari kulipia gharama za kinga kwa wale watu wenye sifa stahiki na zilizo adimu ili wabaki kama hazina kwa jamii."*

*Na. Ally Abbas Yusuph*

## YALIYOMO


- Tahariri Uk.2
- Msomi Gwiji asiyechoka kuthubutu Uk.4
- Kumbukumbu inayokumbusha Mwl.Nyerere Uk. 6-8
- Maoni na Ushairi Uk. 9
- Kumbukizi la Mwanafunzi Uk. 10-11
- Tumkumbuke Chachage Uk. 12

**ARDHI NI UHAI ni jarida la Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa Haki za Ardhi (HAKIARDHI), ambalo hutolewa mara tatu kwa mwaka.**

Kusudi kubwa ni kuwapa wadau wa Taasisi hii taarifa mbalimbali zinazohusiana na mambo ya ardhi.

**Mhariri**
Yefred E. Myenzi

**Bodi ya Wahariri**
Ng'wanza Kamata - M/Kiti
Abdallah Matata - Mjumbe
Rehema Mfaume - Mjumbe

**Mchapishaji**
Alice Shamge

## UJUMBE WA BODI KWA WASOMAJI

WASOMAJI wa jarida hili mnakaribishwa kutoa michango yenu kwa kuuliza maswali, ushauri, maoni au kwa kuandika makala. (zisizozidi kurasa tatu) zitumwe kwa Mhariri kupitia anuani zifuatazo:

Mhariri:
**ARDHI NI UHAI**
**S.L.P 75885**
**Dar es salaam**

Email:
**info@hakiardhi.org**

**Mchapaji**
Ecoprint Ltd.

Email:
**ecoprint@bol.co.tz**

# TAHARIRI

## KUMBUKIZI YA CHACHAGE ITUSAIDIE KUENDELEZA VUGUVUGU LA KIJAMII

Mwezi Mei mwaka 2005, Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa masuala ya ardhi iliandaa kongamno la kitaifa juu ya harakati na mapambano ya umma dhidi ya mifumo kandamizi ambalo lilifanyika katika ukumbi wa baraza la maaskofu Katoliki kurasini jijini Dar es salaam. Kongamano hilo liliwashirikisha wananchi wa kawaida kutoka sehemu mbalimbali za nchi na baadhi ya watetezi wa maslahi ya wanyonge kutoka nchi za Kenya, Uganda na Zimbabwe. Mada mbalimbali ziliwasilishwa na uzoefu wa kila namna ulishirikishwa kutoka kwa wazalishaji wadogo wakiwemo wafugaji, wachimbaji, waokusanyaji na wavuvi. Ujumbe uliotawala siku mbili zote ulibeba vilio, simanzi, majonzi na malalamiko ya wananchi hao zaidi ya miamoja toka karibu kila pembe ya nchi juu ya dhuluma, uonevu na unyayasaji unaoafanywa na watendaji katika dola, wawekezaji na wananchi wenzao wenye vipato vikubwa ambao ama huwafukuza kwenye ardhi yao, machimbo yao, mialo yao, fukwe zao na mapori yao bila fidia au kwa fidia ndogo isiyoendana na hali halisi wala mahitaji yao.

Ndipo akasimama marehemu Profesa Chachage na kutoa changamoto iliyobadili mwelekeo mzima wa kongamano lile. Profesa akawaambia washiriki kuwa maovu katika jamii ya kitanzania yataendelea milele endapo watanzania waliopata mwanga kuhusu hali hiyo hawatasimama kidete na kujitoa mhanga kupigania haki kwa pamoja. Wazo la kuibuliwa kwa vuguvugu la kitaifa la kijamii ambalo hujengwa katika misingi ya hisia za utaifa, uzalendo, uhuru kamili, umoja na mshikamano wa kweli baina ya wanaonyanyaswa na kuonewa likaibuliwa na kujadiliwa kwa kina. Kwa maneno ya profesa Chachage, vuguvugu la kijamii huibuliwa na kila anayejitambua na kutambua kuwa hali fulani au mfumo wa maisha na mahusiano ya kijamii uliopo haufai wala hauwanufaishi walio wengi na hivyo kudhamiria kwa dhati kupambana ili kubadilisha hali hiyo.

Ujumbe huu wa marehemu Chachage natamani uwe ndio msingi na mwongozo wa tafakuri juu ya mustakabali wa taifa letu katika nyanja zote nchini kote. Mjadala kuhusu dhima ya maarifa katika kuleta mabadiliko ya kijamii ni wa muhimu kuliko inavyoweza kuelezeka. Kama aina ya elimu inayotolewa na hata mazingira inamotolewa havitamwezesha mtoto wa kitanzania kuwa na fikra za kizalendo, kuipenda nchi yake, kuipigania na kuhakikisha haki inatendeka, basi elimu hiyo haina msaada wowote kwa jamii ya kitanzania. Elimu ndio chachu ya mabadiliko ya kila kitu kuanzia maendeleo ya juu kabisa ya kisayansi hadi mahusiano ya kijamii ya kawaida. Bila shaka katika dunia ya sasa na hata katika nchi yetu ambapo sauti za wanyonge zinazidi kudidmizwa na wenye uwezo wa kifedha, mtaji, mali na nafasi zao katika jamii, harakati za kupigania haki, usawa, rasilimali za taifa na utu wetu zinapaswa kuwa sehemu ya maisha ya kila siku. Umoja wetu unazaa vuguvugu kila mtu kwa nafasi yake. Harakati za wanafunzi wa chuo kikuu ziungwe mkono na wachimbaji wadogo wa Mererani na zile za wafanyakazi wa shirika la reli na TANESCO. Lakini kila mtu akisimama peke yake tutazidi kuwa mashahidi wa uporaji wa rasilimali zetu huku tukilalamika au kupanga *wei fowadi* kwenye vyumba vya mikutano mwaka hadi mwaka. Jamii yetu itakuwa tu ya tofauti pale ambapo wachache wanaopata maarifa wanayatumia kwa manufaa ya jamii kama alivyofanya ndugu yetu marehemu Profesa Chachage. Tunapomkumbuka leo baada ya mwaka mmoja tuanze na hili la kujaliana na kuthaminiana huku tukiunganisha nguvu zetu pamoja kama vuguvugu la kijamii.

# CHACHAGE YU KATI YETU JAPO HAONEKANI

Inatoka uk. 1

haki na usawa wa binadamu, alitwaliwa julai tisa mwaka jana na kutuachia hazina ya machapisho, hotuba, makala za magazeti, kaseti za redio na luninga na mengine mengi ambayo si rahisi kusahaulika mara moja kwa yeyote anayeamini katika aliyoyasimamia ndugu yetu Chachage.

Hadi mauti inamkuta Chachage alikuwa profesa wa masuala ya kijamii wa chuo kikuu cha Dar es salaam lakini siku ya kutoa salamu za mwisho katika ukumbi wa Nkrumah, mwombolezaji mmoja alisikika akisema huyu hakuwa tu mhadhiri wa chuo kikuu bali wa jamii ya watanzania wote. Hii inatokana na ukweli kuwa alifanya utafiti wa kutosha wa masuala yanayoigusa jamii kama vile ukosefu wa huduma za afya, elimu duni, miundo mbinu hafifu, rushwa, maslahi duni katika ajira, bei duni za mazao ya wakulima na mengineyo mengi ya kijamii na kutumia nafasi yake kuyachambua kitaalamu na kuyawasilisha kwa lugha rahisi tena iliyozoeleka na jamii inayokusudiwa. Hili lilimfanya awe mwanajamii zaidi kuliko kuwa msomi aliyejifungia katika eneo lake la kazi.



*Mzee Ally Abas Yusuph wa Rufiji ambaye ni mwanachama wa HAKIARDHI akimsikiliza kwa makini Profesa Chachage (hayupo pichani) wakati wa Kongamano la ardhi lililofanyika TEC-Kurasini mwaka 2005. Kushoto kwake ni washiriki wengine wa Kongamano hilo Sheikh Gorogosi wa BAKWATA na Gambaseni Dutu wa Meatu Shinyanga*

### Mtu wa Msimamo

Kama kuna jambo lilimkera marehemu Profesa Chachage na ambalo hakuacha kulisema hata siku moja ni mfumo wa kibeberu. Mfumo huu ambao umejengwa katika misingi ya unyonyaji na mahusiano yasiyozingatia haki na usawa katika kupata, kumiliki na kutunia rasilimali umeendelea kumkandamiza mwanancahi wa Tanzania kwa njia mbalimbali zikiwemo uwekezaji, ubinafsishaji wa mashirika ya umma, uchangiaji wa gharama za huduma za kijamii kama vile elimu na afya na kuporomoka kwa uzalishaji kutokana na serikali kuondoa ruzuku katika pembejeo za kilimo. Huku akitambua na kuyaunganisha kwa umahiri mkubwa hayo yote na sera za kimagharibi zinazosukumwa na fuko la fedha la kimataifa (IMF) na benki ya dunia pamoja na mataifa ya kimagharibi na Marekani, Chachage alisimama kidete kukemea, kulaani na kukejeli sera na mfumo huo kwa ujumla akisema zinamfukarisha mwanachi wa kawaida na kurushu uporaji wa rasilimali za nchi kama madini, wanyamapori, misitu na ardhi. Mwaka 2001, alifanya utafiti kuhusu uzalishaji na soko la zao la korosho kwenye mikoa ya kusini mwa Tanzania na kutoa taarifa ya utafiti iliyoonyesha kuwa wananchi wa maeneo hayo walikuwa wananyonywa na makampuni binafsi ya kununua korosho kupitia bei ndogo na ruzuku za pembejeo.

### Jasiri

Profesa Chachage hakuwa na mipaka katika kusimamia ukweli anaouamini jambo ambalo watu wengi limewashinda wakaishia kuwa wanafiki ili kulindiana heshima. Yeye alikosoa hadharani, katika vikao, kwenye vipindi vya redio na luninga na hata ukiwa naye uso kwa uso. Alikosoa serikali na kuisifia pale ilipofanya vizuri. Hali kadhalika, pamoja na kufanya kazi kwa karibu sana na NGOs nyingi hakusita kuzikosoa hasa pale zilipoonyesha ubabaishaji au kutokuwa na msimamo juu ya wanachokiamini. Aliziita kwa majina NGOs za mtindo huo kama vile Next Governemnt Officers au Nothing is Going On. Hii haikuwa na maana kuwa alizichukia NGOs lakini alikuwa na lengo la kuonyesha kuwa NGOs nyingi zimeundwa kwa malengo ya kuendeleza agenda za kibeberu kwa kuchukua sauti na nafasi za wanyonge badala ya kutetea maslahi na rasilimali za wanyonge hao. Mwaka 2004, alialikwa kuhudhuria mkutano mkuu wa HAKIARDHI uliofanyika Zanzibar. Katika mjadala wa bunga bongo ambao wanachama huutumia kijitafakari na kutathmini mchango wao katika jamii kwa mwaka husika, Chachage aliweka wazi msimamo wake kuwa asasi nyingi za kiraia zimeundwa wa watu wa tabaka la kati ambao kimsingi wanatanguliza maslahi yao binafsi huku wakisingizia kutetea wanyonge kama vile wafugaji, waathirika wa UKIMWI, watoto yatima, wajane, au zile za mazingira, afya ya mwanamke na nyanja nyinginezo. Akaonya kuwa asingependa HAKIRDHI iwe miongoni mwa asasi kama hizo kwani alikubaliana na msimamo wake na masuala inayoyashughulikia katika jamii.

### Mtetezi wa Wanyonge

Ukiacha chuo kikuu cha Dar es salaam, ambapo mara kadhaa alisikika akikosoa waziwazi maamuzi ya uongozi wa chuo kuhusiana na uamuzi uliokuwa ukiwaathiri wanafunzi, Profesa Chachage alikuwa msitari wa mbele kutetea makundi mbalimbali ya kijamii hasa wazalishaji wadogowadogo. Alipinga kwa nguvu zote kuwaondoa wachimbaji wadogowadogo wa madini huko Kahama, Geita, Nzega na Mererani huku akisisitiza kuwa mtu hashibi fidia ya pesa ajapopewa mamilioni.

Wamachinga walipoondolewa mara kwa mara kwenye maeneo ya jiji la Dar es salaam pia aliwatetea kwa nguvu zote

Endelea Uk.5

## KUMBUKIZI YA MWALIMU MWENZAKE

# PROFESA CHACHAGE MSOMI GWIJI ASIYECHOKA KUTHUBUTU

*Na Joachim Abnuwas Mwami*

Kwa mara ya kwanza nilionana na marehemu Profesa Chachage mwishoni mwa miaka ya themanini mara tu baada ya kuhitimu masomo yake ya uzamivu katika Chuo Kikuu cha Glasgow, nchini Uskotishi. Siku hiyo tulikuwa tumekusanyika msibani nyumbani kwa kamaradi mwenzetu aliyekuwa amefiwa na mama yake. Kwa takribani saa moja mjadala uliokuwa umetawala miongoni mwa waombolezaji ni suala la mageuzi ya kisiasa na pale nilipojiunga na idara ya Sosiolojia na Anthropolojia ya Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam nikiwa Mhadhiri pamoja naye.

Sio rahisi kuelezea kwa kina sifa za marehemu Chachage kwani ni nyingi na hapa nitajikita katika kuelezea sifa kuu mbili tu. Sifa ya kwanza ni usomi wa vitabu na maandiko mengine. Chachage alikuwa akisoma kitu chochote kile kuanzia Koran, Biblia, historia ya dunia kwa ujumla, jiografia na kadhalika: hakuacha kusoma kitu chochote kilichokuwa zaidi.

Sifa ya pili ya marehemu Chachage ni ile ya kutetea wanyonge wa aina yoyote na mahali popote walipo. Maandiko yake yote yamejikita katika kuchambua kiyakinifu mahusiano ya kijamii, nguvu za kitabaka ikiwa ni pamoja na michakato ya kijamii iliyopo nchini Tanzania ambayo ndiyo chanzo cha matatizo yote ya kijamii yaliyopo Tanzania. Kwa mfano, maandiko yake ya ufukarishwaji wa wachimbaji migodi wadogo wadogo wa madini; ufukarishwaji wa wakulima na wafugaji wadogo wadogo n.k. yote yakiwa yamejikita katika kuonesha aina ya mahusiano ya kinyonyaji na kikandamizaji yanayojengwa na mabepari uchwara wa ndani na mabeberu wa nje yanavyosababisha umaskini miongoni mwa Watanzania wengi licha ya rasilimali zilizopo. Na hapa tukumbuke kwamba tafsiri yake ya **utandawazi** kama **utandawizi** ndipo inapokuwa na mantiki.



Dr. Joachim Mwami akichangia mada katika mojawapo ya mikutano ya HAKIARDHI ambayo Profesa Chachage alikuwa mhusika mkubwa.

Mwisho, katika miaka yote ambayo nimekuwa nikifanya kazi na marehemu Chachage, nilivyomwelewa mimi, ni kwamba alikuwa mcheshi, mwema, na mkarimu sana lakini jasiri wa kuweza kusema kitu kile alichokuwa anakiamini. Nimepewa taarifa ya kuandaa kumbukizi hii kwa muda mfupi na pia kujulishwa kuwa nafasi ya kuandika mengi isingekuwepo hivyo nafurahi kuona kuwa baada ya mwaka mmoja watu wenye moyo kama wa Chachage wanakumbuka hata kuandaa vitu kama jarida hili ili watoto wetu na hata wajukuu wetu wakue wakielewa kuwa kuna watu kama Chachage walioacha usomi wao pembeni wakajitoa mhanga kupigania wanyonge bila kujali hadhi na hali zao.

kiuchumi yaliyokuwa yameanzishwa na serikali ya Rais Mwinyi kwa shinikizo la vyombo vya kibeberu ( Benki ya Dunia na Shirika la Fedha Duniani) na hatma ya nchi yetu.

Uchambuzi yakinifu aliotoa marehemu Chachage ndio uliovutia zaidi na hasa uwezo wake wa kusema haraka haraka ikiwa ni pamoja na kubadilisha maana ya msamiati kutoka kwenye ile maana iliyozoeleka. Kuanzia hapo ndipo nikaanza kumwelewa marehemu Chachage na niliendelea kuwa karibu naye na baadaye tukawa marafiki hasa mbele yake. Chachage aliamini kwamba ili mapinduzi ya kijamii yaweze kutekelezwa, wanamapinduzi ni lazima wasome kila aina ya maandiko hata yale yanayoandikwa na adui zao kwani "utawezaje kupigana na adui yako ikiwa humfahamu?": hili ndilo lilikuwa ni dokezo lake kila mara. Mara nyingi alikuwa akisononeshwa sana na hii tabia ya watanzania, hasa vijana wetu kutopenda kujisomea; kwani kwa mtindo huu, watanzania tunakaribisha kutawaliwa kimawazo/kielimu na hivyo kuendelea kuruhusu mabeberu kuendelea kututawala

# ... YU KATI YETU JAPO HAONEKANI

*Inatoka uk. 3*

akibainisha kuwa wengi wao ni matokeo ya sera mbovu na mfumo usiowajali wananchi wake kwani mfumo wa uzalishaji mali umewatupa nje ili kuwaruhusu wachuuzi wa kigeni kugawana rasilimali za nchi.

**Msomi na mwandishi**

Kwa upande wa elimu, marehemu Profesa Chachage alikuwa msomi aliyebobea katika masuala mbalimbali. Licha ya kujielimisha hadi kiwango cha juu kabisa cha elimu yaani udaktari wa falsafa kwa masuala ya kijamii, haikuwa rahisi sana kwa mtu asiyemjua vizuri kufahamu hasa amesomea mambo gani kutokana na kumudu masuala mengi ya kijamii, kiuchumi, kisheria, kisiasa, kiutamaduni na nyanja nyingine nyingi. Alipenda kusoma, kufanya utafiti na kuandika na ndiyo maana aliweza kuandika machapisho zaidi ya tisini katika muda ambao wahadhiri na watu wengine wengi waliofanya nae kazi katika kipindi cha uhai wake hawajaweza kufikisha hata robo tu ya kazi zake.

Profesa Chachage aliacha hazina ya vitabu vyenye ujumbe adhimu sana ambao kwa wasomaji wazuri watakiri kuwa ni wa wakati wote na kwa watu wa takribani rika zote. Riwaya ya Sudi ya Yohana ni fupi na inatumia lugha rahisi ambayo hata watoto wanaweza kuisoma kama hadithi ya kawaida japo imejaa ujumbe mzito na fikra za kiukombozi. Kadhalika lugha iliyotumika katika riwaya kama ya makuwadi wa soko huria inavutia kusoma huku ikiwasilisha ujumbe mzito kuhusu uhusika wa watendaji wenye dhamana ya kulinda rasilimali za nchi kwenye mnada wa kuziuza rasilimali hizo kwenye soko huria huku wakiipiga kumbo dhamana yao ya kuzilinda kwaniaba ya wananchi wote. Katika magazeti, Profesa Chachge aliandika makala nyingi ikiwemo kolamu kubwa katika gazeti la mtanzania ikielezea historia ya vita vya majimaji ambayo binafsi niliifuatilia na ikanikumbusha mambo mengi ya kihistoria ya nchi yetu. Aina hii ya uandishi inamtambulisha mtu wa kipekee kwa jamii anayoikusudia kwani angeweza kutumia lugha ngumu inayolenga tabaka fulani tu la wasomaji jambo ambalo Chachage hakufanya hivyo.

**Mwanaharakati Mwanamapinduzi**

Mwaka 2004 alihudhuria jukwaa la kijamii la kidunia huko Mombai India ambapo asasi mbalimbali za kijamii na watetezi wa masuala ya haki duniani kote hukutana kujadiliana na kupanga mikakati ya kuboresha mahusiano ya kidunia ili kuleta usawa kwa makundi ya watu mbalimbali. Alipotoka huko alifanya tathimini na kusema wanaharakati wengi hutumia nafasi hiyo kuendedeleza mifumo kandamizi na kujinufaisha kwa kutumia majina ya wanyonge. Badala yake akahimiza kuwa na majukwaa ya kijamii ya wanamapinduzi ambao wanasukumwa na dhamiri ya ukombozi wa kweli wa jamii zinazokandamizwa kama vile za wafugaji, mama lishe, vibarua wa viwandani, migodini, wachuuzi na makundi mengine ya aina hiyo. Dhamira hii ndiyo unakutana nayo unaposoma machapisho yake kama Almasi za Bandia, Makuwadi wa Soko Huria, Sudi ya Yohana na hata michango iliyo katika makala za magazeti, majarida ya kimataifa na vitabu vyake au alivyohariri na kuchangia makala.

**Mwanajamii**

**Sisi leo tuko wapi? Je tuna uwezo hata wa kutoka nje ya ofisi au nyumba zetu kumtetea mmachinga anayebomolewa kibanda kupisha mwekezaji? Au ni makuwadi tunaokimbia huku na kule kutafuta na kutoa ushauri welekezi na kuonyesha ilipo ardhi ya vijiji yenye rutuba apewe mwekezaji bure! Mbio alizoanzisha Chachage lazima ziendelee na wa kuziendeleza ni sisi tulio hai tunaoamini katika nyendo zake.**

Maisha ya kijamii ya Chachage pia yaliacha chamgamoto kubwa miongoni mwa wasomi na watu wa kawaida. Kwa kiwango chake cha elimu na hadhi yake kama Profesa katika chuo kinachoheshimika nchini isingekuwa ajabu kwake kujitenga na jamii ya kawaida kama ilivyo kwa watu wa hadhi yake. Lakini chachage alijichanganya na watu wa makundi mbalimbali katika jamii kuanzia majirani zake eneo la Changanyikeni alikoishi, vijana wa marika mbalimbali, wasanii wa muziki na fani nyinginezo, wanafunzi wa chuo kikuu na sekondari na wahadhiri wenzake chuoni. Pia alikuwa daraja kati ya wahadhiri wa idara mbalimbali kupitia umoja wao wa UDASA jambo ambalo wahadhiri wenzake wengi walikiri umahiri wake wa kuwaunganisha hata waliokuwa wameona UDASA ni chombo kisicho na maana kwao.

Ukiacha maeneo ya Chuo kikuu Profesa Chachage alifanya kazi kwa karibu na asasi nyingi za kiraia zinazojishughulisha na masuala ya kijamii bila kubagua aina wala hadhi ya asasi hizo. Alikuwa msitari wa mbele kushiriki shughuli mbalimbali za mashirika kama Mtandao wa Jinsia Tanzania, HAKIARDHI na mengine mengi. Katika Mtandao wa Jinsia Chachage alishiriki kwenye matamasha ya jinsia ambayo huandaliwa na shirika hilo kila baada ya mwaka mmoja ambapo alikuwa akiwasilisha mada mbalimbali, kuandika makala na kuhariri machapisho yao. Mwaka 2005, aliratibu na kuongoza mijadala juu ya mustakabali wa rasilimali za taifa akiwasilisha mada iliyotokana na utafiti kuhusu mchango wa sekta ya utalii kwenye uchumi wa taifa.

Kwa upande wa shirika la HAKIARDHI Profesa Chachage, alishiriki katika upangaji wa mipango ya shirika kama mshirika wa karibu, kwenye makongamano ya kitaifa juu ya ardhi na rasilimali na shughuli za vijijini. Pia aliwasilisha mada na kuongoza mijadala kwenye semina za kila mwezi na hadi mauti inamkuta alikuwa katika maandalizi ya kulifanyia tathmini ya kina shirika la HAKIARDHI baada ya kukamilisha programu zake za miaka sita vijijini. Ndani ya shirika, alionekana kama mfanyakazi, mwanachama na kiungo muhimu kati ya watendaji na washirika wengine ndani na nje ya shirika.

Nihitimishe kwa kusema kuwa, hakuna namna yoyote ambayo tunaweza kujiridhisha kuwa tunamuezni ndugu yetu tuliyempenda sana marehemu Profesa Chachage kama hatutatimiza wajibu wetu kwa vitendo iwe kwa kutafiti, kujiendeleza kielimu ili kupata maarifa ya kweli, kuwa na msimamo na kukemea na kukosoa kwa ujasiri maovu yanayoiangamiza jamii na kupigania usawa na haki kwa wote. Chachage alijitanabaisha na kundi la watu wanyonge, watu wasio na sauti katika jamii na kujitoa mhanga kuwapigania kwa kalamu na vitendo. Kutoka maghorofa ya chuo kikuu, aliteremka hadi Kazimzumbwi, akawatetea waliochomewa nyumba na dola, akaenda Newala kutetea wakulima wa korosho wanaolanguliwa na mabepari uchwara matajiri, akafika Manyara na Ngorongoro kutetea ardhi ya malisho ya wafugaji na kule Rufiji kutetea waathirika wa mradi wa kamba. Sisi leo tuko wapi? Je tuna uwezo hata wa kutoka nje ya ofisi au nyumba zetu kumtetea mmachinga anayebomolewa kibanda kupisha mwekezaji? Au ni makuwadi tunaokimbia huku na kule kutafuta na kutoa ushauri welekezi na kuonyesha ilipo ardhi ya vijiji yenye rutuba apewe mwekezaji bure! Mbio alizoanzisha Chachage lazima ziendelee na wa kuziendeleza ni sisi tulio hai tunaoamini katika nyendo zake. Tukielekeza jitihada zetu katika kupigania haki kwa wote, tutakuwa tunamuenzi mwenzetu, mpiganaji jasiri wa haki na utu wa binadamu ambaye yu kati yetu japo haonekani kwa aliyoyafanya na kutuachia. Tutakiane heri katika kuyaendeleza majukumu hayo mazito.

# PROFESA CHACHAGE: KUMBUKUMBU INAYONIKUMBUSHA MWALIMU NYERERE

*Na Mathew Agripinus Senga*

Hapana shaka hata kidogo kuwa kuna mambo mengi ambayo aliyekuwa mkuu wa idara ya Sosiolojia na Anthroplojia, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Hayati Profesa Chachage Seithy Loth Chachage alishabihiana sana na Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Ninazo sababu lukuki za kusema hivyo, lakini kubwa ni kwamba, ninapokumbuka uwezo mkubwa aliokuwa nao Mwl. Nyerere najikuta nikikumbuka pia umahiri aliokuwa nao Profesa Chachage, si tu katika kuchanganua mambo kwa kina, bali katika kuonesha uzalendo kwa nchi yetu ya Tanzania.

Mwl. Nyerere alikuwa na sifa nyingi. Nia yangu si kurudia sifa za Mwl Nyerere, lakini najaribu kuonesha namna ambavyo uwezo wa Baba wa Taifa utabakia katika historia ya vizazi na vizazi hapa duniani. Kwanza kabisa Mwl. Nyerere alikuwa mwalimu hasa, mwalimu ambaye wanafunzi wake wanajisikia faraja kufundishwa naye. Mwalimu ambaye ni makini awapo ndani na nje ya darasa. Mwalimu ambaye yupo tayari kumsaidia mwanafunzi kuelewa kinachotakiwa, ili na yeye asaidie wanafunzi wenzake anapokosekana. Zaidi Mwl. Nyerere alikuwa mwalimu ambaye anaona uchungu pale anapogundua kuwa mwanafunzi wake mmoja au wawili watatu hawamwelewi kutokana na sababu mbalimbali zinazotakana na udhaifu wao. Tumesoma na kusikia habari nyingi za watu ambao walitokea kufundishwa na Mwl. Nyerere, wakielezea jinsi ambavyo alikuwa mwalimu makini na anayejituma katika kipindi chake cha utumishi wa serikali kama mwalimu.

Yeye binafsi alichukia tabia ya walimu kutokuwa makini. Mfano mzuri ni pale alipotoa hotuba katika Chuo cha Ualimu Morogoro, Agosti 27, 1966 ambapo alionesha kukerwa na walimu wasiokuwa makini. Mwalimu Nyerere alisema kuwa, inapotokea mwalimu anaingia darasani amechoka au mwenye kuonekana kuchoka, aliyevunjika moyo na asiye na hamu ya kazi na ambaye anahitaji kila kazi ifanywe na wanafunzi huku yeye akiangalia, au ambaye anawaona wanafunzi kama wanamchosha, inapotokea hivyo wanafunzi watajenga mawazo kuwa ualimu ni kazi ya kuikwepa na kwamba kusoma ni kama jambo ambalo mtu anapaswa kupitia tu na pia njia ya kutumia mamlaka ni kuwafanya watu wengine wakufanyie kazi. Hapa Mwalimu Nyerere alikuwa akionesha kuwa waalimu wana nguvu zaidi ya watu wengi wanavyoelewa, na kwamba wana ushawishi mkubwa katika jamii kama tokeo la ushawishi huo kwa wanafunzi wao.

Sifa hii ya Mwl. Nyerere ndiyo inayonifanya pia nijaribu kufananisha na ile aliyokuwa nayo Profesa Chachage, ya "ualimu makini". Kama alivyokuwa Mwl. Nyerere, Profesa Chachage alikuwa Mwalimu makini, anayejituma, na mwenye uchungu na kazi yake. Bahati nzuri nilitokea kuwa mmoja wa wanafunzi wa Profesa Chachage kuanzia masomo yangu ya shahada ya kwanza na ile ya uzamili katika sosholojia. Hapa ndipo nilipoweza kuona umakini wa Mwl. Nyerere kupitia yeye. Profesa alipenda kila mwanafunzi wake aelewe, na alipojua kuwa hujaelewa ni lazima utagundua ni jinsi gani alikuwa akijisikia uchungu, uchungu wa kuona kwa nini humwelewi. Tumeelezwa kuwa darasa la Mwl. Nyerere lilikuwa linawajibika kujiandaa kabla hajaingia ili kuweza kukabiliana na changamoto mbalimbali ambazo alikuwa akizitoa kwa wanafunzi wake. Hali hiyo ndiyo iliyokuwa ikitukuta sisi tuliokuwa wanafunzi wa Profesa Chachage. Ilikuwa ni vigumu kwa mwanafunzi kujisikia amani moyoni kama anajijua kuwa hajajiandaa. Ukiulizwa swali na Profesa ni lazima uhakikishe ya kuwa utakachojibu ni lazima umekisoma na hata kukifanyia utafiti wa kina. Ilikuwa si rahisi kumdanganya Profesa, kama ambavyo haikuwa rahisi kumdanganya Mwl. Nyerere. Hii inaonesha kuwa walimu hawa wawili walikuwa wanatumia muda wao si kwa ajili ya kufundisha tu, bali pia kuongeza ujuzi wa mambo mbalimbali yanayohusiana na kile wanachokifundisha.



'Profesa Chachage akiwa nje ya Ukumbi wa Baraza la Maaskofu Katoliki wakati wa Kongamano la Kitaifa la Masuala ya Ardhi mwaka 2005*

Hivi leo ni walimu wangapi ambao wana sifa kama hizo? Asilimia kubwa ya walimu waliopo sasa wanachojua kuwa ni jukumu lao ni kufundisha, tena kufundisha kwa mtindo wa kuwasomea wanafunzi notisi zilizoandaliwa miaka na miaka. Mwalimu kazi yake kubwa inakuwa ni kusubiri muda wa kipindi na kutafuta alichowafundisha wanafunzi wake wa mwaka uliopita, na kwenda kukitoa kama kilivyo darasani. Mwalimu haanzishi mada zinazochangamsha darasa kujadiliana masuala mbalimbali. Kibaya zaidi ni kwamba, anachelewa darasani kwa dakika kumi na anawahi kutoka dakika kumi na tano kabla muda haujaisha. Lakini ni mwalimu huyu huyu ambaye haishi kulalamika kuwa wanafunzi wa siku hizi ni wagumu kuelewa, wavivu na hawana tabia ya kujisomea na kuchunguza mambo kwa kina. Hali hii ni tofauti kabisa na ile aliyokuwa nayo Mwl. Nyerere na Mwl. Profesa Chachage. Nafikiri wakati umefika wa walimu kuiga mwenendo wa walimu hawa mahiri ili kujenga kizazi bora cha watanzania makini, wenye tabia ya kujisomea na kutafiti mambo kwa kina na kisha kuyatolea ufafanuzi. Hii itasaidia pia kujenga uzalendo kwa nchi yetu katika zama hizi ambazo Mwl. Nyerere na Profesa waliziita kwa majina tofauti lakini yenye maana zinazofanana, 'ukoloni mambo leo' na 'utandawizi'.

Mwalimu Nyerere alikuwa kiongozi thabiti. Sifa za uongozi za mwalimu ni vigumu kuzielezea kwa uhakika. Mwl. Nyerere alikuwa miongoni mwa viongozi wachache wa kutolewa mfano, si tu katika bara la Afrika bali duniani pote. Baba wa Taifa alikuwa na sifa zote za kiongozi thabiti, alikuwa kiongozi anayejituma na aliyejitoa kwa ajili ya nchi yake. Haya yanadhihirishwa na nyadhifa mbalimbali za uongozi ambazo hakuwahi kuziomba au kuzipigania. Mwalimu alikuwa kiongozi wa watu na wao ndiyo waliopenda siku zote awe kiongozi wao. Historia inatueleza kuwa Mwalimu alianza kuwa kiongozi tokea akiwa na umri mdogo katika shule na maeneo mbalimbali aliyopitia. Hii inaonesha kuwa kipaji cha uongozi cha Mwl. kilianza kuonekana mapema miongoni mwa watu



aliokutana nao, na ndiyo maana hawakusita kumpendekeza au kumchagua kuwa kiongozi wao. Kuonesha kuwa alikuwa na uchungu na nchi yake, Mwl. alikubali hata kuacha kazi ya ualimu "wa darasani" ili ashiriiki kikamilifu katika harakati za ukombozi wa nchi yetu ya Tanzania. Mwl. alidhihirisha uthabiti hata alipokuwa Rais wa nchi hii. Tunaelezwa ya kuwa Mwl. alikuwa mwiba mkali kwa watendaji wazembe katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali.





*Profesa Chachage akiwasilisha mada katika mojawapo ya mikutano ya HAKIARDHI*

Sifa za uongozi za Mwalimu Nyerere zilizidi kujidhihirisha hata kwa jirani zetu na nchi nyingine mbalimbali duniani pale ambapo alikubali kuwa kiongozi katika harakati za kupigania uhuru kwa nchi ambazo zilikuwa hazijapata uhuru, na hata kufikia kukaribisha harakati hizo kuanzia katika nchi yetu. Nchi yetu ilikaribisha vyama kama ANC na SWAPO kuifanya Tanzania kuwa makao yao katika kupanga mikakati ya kujikomboa katika makucha ya ukoloni. Hii ni sifa kubwa ambayo kiongozi mwenye kujua maana ya uhuru anapaswa kuwa nayo. Mwalimu aliona mbali, na kila mara alikuwa akiielezea dhana yake kuwa si kitu kwa Tanzania kuwa huru wakati nchi nyingine za kiafrika bado zinatawaliwa. Baba wa Taifa pia hakuyumbishwa na siasa wala vitisho vya nchi zinazojiita zilizoendelea. Alijali dhana ya utaifa na uzalendo katika maamuzi yeyote yaliyogusa maslahi ya wananchi. Ni viongozi wachache mno ambao wana upeo na mtazamo kama wa mwalimu. Tunayo shuhudia leo kwa viongozi wengi wa nchi za kiafrika na nyingine zinazoitwa zinazoendelea ni kuwakumbatia mabeberu wa dunia kwa kigezo cha kuogopa kunyimwa misaada. Sera za mataifa makubwa ndizo bado zinaendelea kupigiwa upatu huku hakuna juhudi zozote miongoni mwa nchi za 'dunia ya tatu' kuonesha msimamo katika maamuzi yanayojali maslahi ya mataifa hayo.

Hili linanifanya pia nimkumbuke Profesa Chachage, uthabiti katika uongozi. Katika kipindi nilichofanya kazi chini yake nikiwa Tutorial Assistant na yeye akiwa mkuu wa idara ya Sosholojia na Anthropologia niligundua mambo mengi kupitia Profesa Chachage. Kama inavyoelezwa na watu waliowahi kufanya kazi chini ya mwalimu Nyerere, Profesa Chachage pia alikuwa kiongozi thabiti, asiyeyumbishwa na asiyetetea uzembe katika kazi. Pamoja na kuwa alikuwa na majukumu makubwa ya kiuelemishaji, lakini Profesa kama ilivyokwa kwa Mwalimu alijituma mno katika kazi, na haikuwa jambo la kushangaza sana kwetu tulipokuwa tukimuona akiondoka ofisini usiku kutokana na majukumu mbalimbali ya kikazi yaliyokuwa yakimkabili. Mbali na ukuu wa idara, Profesa alikuwa ni Mwenyekiti wa Baraza la Wanataaluma wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDASA) na siku zote alijali maslahi ya wafanyakazi wenzake, na si wafanyakazi tu bali hata ya wanafunzi pale ambapo palitokea mvutano kati yao na utawala au serikali. Hali hii ya uongozi makini ambayo alikuwa nayo Profesa Chachage inashabihiana kabisa na ile aliyokuwa nayo Mwalimu Nyerere. Wote alijitoa kwa ajili ya kupigania maslahi ya umma, bila ya kujali rangi, kabila wala dini.

Lakini leo hii tukiangalia, ni viongozi wangapi walio na mioyo kama hiyo? Ni viongozi wangapi ambao wapo tayari kuubaki maofisini wakifanya kazi za ujenzi wa taifa mpaka usiku uliopitiliza? Tunachoshuhudia leo ni majibu kutoka kwa makatibu mahsusi wao kuwa hawapo katika ofisi zao, na unapochunguza kwa makini unagundua kuwa, kutokuwepo kwao ofisini hakusababishwi na kuwa na majukumu ya kikazi nje ya ofisi zao, bali kunatokana na kuwa na majukumu binafsi nje ya ofisi zao katika muda wa kazi. Wengi wamekuwa wakifanya ziara katika vivutio mbalimbali vya watalii, wakijaribu kuiga mfumo wa wenzetu wa mataifa ya magharibi ambao kwao sehemu za kuliwaza mawazo yao baada ya kazi ni katika mbuga zetu za wanyama, na sehemu za kuongeza ufahamu katika kile wanachoamini 'kutokuendelea' kwetu ni kuja kutembea na 'kushangaa' juu ya mfumo wetu wa maisha. Kiongozi ambaye tunategemea yupo ofisini kwa ajili ya kutatua kero mbalimbali za wananchi, au ambaye tunategemea kuwa ndiye anayepaswa akutembelea wananchi kule waliko ili kutatua shida zao, ndiye huyo huyo kiongozi ambaye anaomba muda ukimbie haraka ifikie ule rasmi wa kumaliza shughuli za kiofisi ili aweze kukimbilia kupata 'moja moto moja baridi'! Hapa sina maana ya kusema kuwa viongozi makini hawapaswi kujipumzisha na kuburudika, lakini ninachokiongelea ni ile hali ya kutumia muda ambao ulipaswa kuwa wa kuwatumikia wananchi kwa ajili ya manufaa binafsi. Kwangu hili nalifananisha na unyonyaji na udhalimu mkubwa, kwa kuwa kiongozi amewekwa na wananchi ili aweze kuwatumikia kikamilifu, kutofanya hivyo, si tu ni kuwadhulumu haki zao, bali ni kuwanyonya!

Mwalimu Nyerere alikuwa ni mpenda haki, usawa na amani. Mwalimu hakupenda dhuluma na siku zote alitetea usawa wa binadamu na kupigania amani. Hili tunaliona katika mambo mengi ambayo mwalimu aliyafanya, ikiwemo pia hotuba zake. Nyingi ya hotuba za Mwalimu zimejaa maudhui ya haki usawa na amani. Mwalimu alikuwa mkorofi kwa wale ambao kwa makusudi waliwanyima haki wenzao. Yeye alitaka kila mmoja aweze kupata haki katika nyanja mbalimbali kwani aliamini kuwa haki haikuwa suala la wachache kutokana na kwamba siku zote haki haiuzwi kama vile ambavyo bidhaa zinavyouzwa dukani. Aliamini ya kuwa umoja wa kitaifa unajengwa na misingi ya haki na endapo misingi hiyo itavunjwa au kupindishwa ndiyo mwanzo wa machafuko ambayo ni kikwazo cha maendeleo ya kweli. Mwalimu pia alipenda usawa bila kujali nafasi ya mtu katika jamii. Kwa Mwalimu kila mwananchi alikuwa sawa na mwenzake pasipo kujali cheo au dhamana, uwezo wala rangi yake. Katika makala yake iliyochapishwa katika gazeti la *The Nationalist*, Februari 14, 1967 iliyobebwa kichwa cha habari chenye tafsiri "Ujamaa si ubaguzi wa rangi", Mwalimu alisema kuwa kama sehemu kubwa ya watu katika jamii fulani ni weusi basi watakaofaidika na ujamaa ni weusi, lakini hili haalina maana Endelea Uk.8

# KUMBUKIZI YA MWANAFUNZI

Inatoka uk. 7

katika rangi yao, bali ni katika 'utu' wao. Lakini pia alisisitiza kuwa bila ya kukubalika kwa usawa wa binadamu hakutakuwa na ujamaa. Ingawa katika Tanzania kwa sasa hatuongelei juu ya ujamaa lakini tunapaswa kutambua ya kuwa usawa kwa xwanadamu ni jambo la msingi. Na mara nyingi tunashindwa kutambua ya kuwa, watu wanazungumzia kukosekana kwa usawa na haki katika jamii yetu kwa kuwa tupo katika mfumo ambao suala la usawa halipo.

Hatuwezi kuwa na usawa katika mfumo ambao unaruhusu matabaka, unyonyaji na unyanyasaji miongoni mwa watu. Jambo hili lilimkera sana Mwalimu na hakusita kuliongelea mara kwa mara na kuliunganisha na suala la amani. Hali hii ilisababisha Mwalimu kupewa nafasi ya kuwa kiongozi katika usuluhishi wa migogoro mbalimbali hata mara baada ya kung'atuka na hili lilidhihirishwa na kutetea kwake haki, usawa na amani. Kwa upande wa Profesa Chachage hali ilikuwa hivyo pia. Pamoja na kwamba hakuwa kiongozi wa nchi kama ilivyokuwa kwa Mwalimu Nyerere, Profesa pia alikuwa mtetezi mkubwa wa haki, usawa na amani. Kazi nyingi na machapisho ya Profesa yalisisitiza dhana hizi. Profesa Chachage aliamini ya kuwa hatuwezi kuongelea amani ya kweli kama tunaendelea kuwa na tabaka la watu wanaojilimbikizia mali ambazo wanazipata kutokana na unyonyaji, kunyonya tabaka lisilomiliki njia za uzalishaji. Na mara nyingi alisema kuwa amani tunayozungumzia ni amani ya juu juu (superficial) kwani hata wale ambao wamejilimbikizia mali wanaishi kwa wasiwasi na ndio maana wanaweka vizuizi katika milango yao pamoja na walinzi kwa hofu ya kuvamiwa na majambazi kwa mfano. Tunaona pia ya kuwa Profesa alipenda amani, usawa na haki na hili linathibitishwa na kufikwa na umauti wakati akiwa katika kazi aliyopewa ya kuratibu maoni ya Muungano.



*Marehemu Profesa Chachage akisisitiza jambo katika Kongamano juu ya harakati na mapambano ya umma katika ukumbi wa TEC-Kurasini Dar es Salaam-Mei 2005*

Mitazamo ya Mwalimu Nyerere pamoja na Profesa juu ya masuala ya haki, usawa na amani inashabihiana. Lakini yatupasa tujiulize jambo moja, amani, usawa na haki vinavyohubiriwa leo hii na wengi miongoni mwa viongozi wetu vinatoka katika mioyo yao kwa dhati? Ni viongozi wangapi ambao wanahubiri usawa, haki na amani katika majukwaa na mikutano mbalimbali lakini wao wakiwa wamejilimbikizia mali, wakiendelea kuwanyonya walala hoi na hata kuwanyanyasa? Ni wangapi ambao kwa makusudi wamekuwa wakitumia nyadhifa zao na madaraka katika kuwakandamiza wanyonge wanaodai haki zao. Sote tunategemea ya kuwa vyombo vya dola na vya kisheria ndio mahali pa kukimbilia pale ambapo haki inakosekana, lakini tumesikia mara ngapi malalamiko ya watu kutotendewa haki katika vyombo hivyo? Mlinda sheria ndiyo anakuwa mvunja sheria, wapi basi raia wanyonge wasio na fedha wala madaraka waende kwa ajili ya kupata haki zao?

Mwalimu Nyerere alichukia sera kandamizi na mifumo ya kibepari na kibeberu. Mwalimu aliamini kuwa ni vigumu kwa wananchi kujikwamua katika hali ngumu kiuchumi kama mifumo ya kinyonyaji itaendelea kujikita katika nyanja mbalimbali za maisha yao. Hakusita wala kuwaonea haya mabeberu ambao kupitia sera kandamizi walizoziandaa wanafikiria njia za kukusanya utajiri kinyonyaji kwa vigezo vya misaada na soko huria. Mwalimu hakupenda kabisa ubinafsishaji wa mashirika na taasisi za umma na alikuwa akitamka wazi kabisa kuwa kufanya namna hiyo ni kukaribisha matabaka na kuruhusu kupenya kwa mirija ya unyonyaji, vitu ambavyo havishabihiani na haki, usawa na amani. Hata alipokuwa katika ziara mbalimbali katika mataifa ya nchi zinazojiita zimeendelea, mwalimu hakusita kuwapa 'vidonge' vyao. Aliwaeleza wazi jinsi ambavyo tawala na sera zao dhalimu hazikuwa na maana kwa maendeleo ya bara letu na nchi zetu kwa ujumla. Mwalimu hakuwa msemaji wa nchi ya Tanzania peke yake, bali alikuwa kinara wa nchi zote zilizogubikwa na unyonyaji unaofanywa kwa kigezo cha maendeleo na mataifa hayo 'teule'. Hakusita pia kkuelezea athari za utandawazi na kuwataka wananchi kuwa makini nao.

Mtazamo na fikra za Mwalimu katika kuchukia mifumo hiyo havikutofautiana na Profesa Chachage. Profesa alipinga kwa nguvu zake sera za utandawazi ambao aliubatiza kwa jina la 'utandawizi' na aliona kuwa sera hizo ndizo zinazoletelezea umaskini mkubwa katika 'nchi za dunia ya tatu'. Mfano mzuri ni katika moja kati ya kazi zake iliyochapishwa katika kitabu cha *Globalisation and Social Policy in Africa* kilichoandaliwa na CODERSRIA (Council for the Development of Social Science Research in Africa), yenye kichwa cha habari chenye tafsiri ya "Hitimisho- Ajenda ijayo: Zaidi ya Utandawazi", Profesa Chachage alieleza kuwa kwa njia moja au nyingine utandawazi ndio umekuwa chanzo cha watu kupata huduma za kijamii na kukosa kazi. Alisema pia kuwa utandawazi umewatupa watu katika shida na matatizo makubwa yasiyoweza kuvumilika. Usadifu huu wa mawazo na fikra juu ya mifumo hii kandamizi umeshabihiana sana na ule wa Mwalimu Nyerere. Tukiangalia kwa umakini, matatizo mbalimbali ambayo jamii yetu inakabiliana nayo kwa sasa, chanzo chake ni mifumo hii ambayo 'manabii' haw walikuwa wakiipigia makelele waziwazi na kukuchukizwa nayo. Kinachotokea kwa sasa ni kunyamaza kimya kwa kuogopa kunyimwa misaada na mataifa haya huku tukijua fika ya kuwa tunaumia. Sifahamu hali hii itaendelea mpaka lini, lakini nafikiri kuwa hatuna budi kuiga mfano wa Mwalimu, Profesa na baadhi ya viongozi kama Hugho Chavez wa Venezuela na Fidel Castro wa Cuba ili tusikubali kuuza 'utu' wetu.

Bado kuna maeneo mengi ambayo Mwalimu Nyerere na Profesa walifanana. Nia ya makala hii si kuyazungumzia yote lakini ni kutoa changamoto kwa wasomi na viongozi waliopo sasa. Kazi kubwa iliyo mbele yao ni kuhakikisa kuwa maslahi ya taifa yanawekwa mbele kwanza na kusahau kabisa maslahi binafsi. Kinachotakiwa hapa ni uzalendo, na si uzalendo wa maneno bali wa vitendo. Tunapokuwa na uchungu na maendeleo ya nchi yetu na kuonesha kwa vitendo ndipo tunaposhiriki kikamilifu katika kusukuma mbele gurumudu la maendeleo. Wasomi watumie nafasi zao katika kufanya tafiti mablimbali zinazogusa maisha ya watu na kuweka wazi kipi kifanyike kwa ajili ya maendeleo ya pamoja. Viongozi wahakikishe kuwa mipango ambayo ina mtazamo wa kitaifa inatekelezwa kwa wakati kwa faida ya wananchi ambao wao ni sehemu yao. Tusiogope kuyumbishwa na wanaojiona wenye nguvu, tuzingatie uzalendo kama ambavyo Mwalimu Nyerere pamoja na Profesa Chachage walivyokuwa wakizingatia. Nia yangu si kusema kuwa hawa wawili pekee ndio walikuwa wazalendo kwa nchi yetu, nafahamu kuwa tunao wengine kadhaa. Lakini kinachotakiwa hapa si maneno bali matendo ya kila mmoja wetu kwa ajili ya faida ya nchi yetu, bila kujali dini, rangi, kabila, jinsia wala umri. Zidumu fikra za muasisi wa Taifa letu Mwalimu Nyerere pamoja na mwanazuoni Profesa Chachage!

**Mwandishi ni Tutorial Assistant katika idara ya Sosholojia na Anthropolojia,**
**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam,**
**e-mail: magripinus@hotmail.com**

MAONI/ USHAIRI

# CHACHAGE AMEUMBIKA!

Na. Deus Kibamba



Hujafa hujaumbika ni msemo wa Kawaida wa Kiswahili. Chachage ameumbika ni msemo wangu mwenyewe! Natamka rasmi kutoka moyoni mwangu kuwa Chachage ameumbika. Ni mwaka hivi sasa tangu ile siku dunia ilipopasuka kusikia habari za Chachage kupumzika. Kama tunavyofahamu, Chachage amefariki, chachage ameumbika!

Nilikuwa nimpigie simu Jumatatu ile, nikiwa ndio nimerejea Jumamosi kutokea Masomoni, Uholanzi. Lengo ilikuwa ni kupanga kukutana ili nijue amefikia wapi na umaliziaji wa kazi ya utafiti juu ya madhara ya Ubinafsishaji Afrika Mashariki na Kusini ambao alikuwa akiendelea nao kwa takribani mwaka mzima. Kabla sijampigia, nikiwa katika kusabahiana na wafanyakazi wenzangu wa Mtandao wa Jinsia tulioonana miezi takribani minne iliyopita, nilipata ujumbe wa kufariki kwa profesa, daktari, mwalimu, mwanafalsafa, mwanamapinduzi, mtaalamu, mchambuzi, mwandishi, msanii na mwanahabari, Seithy L. Chachage. Hujafa hujaumbika, Chachage akawa amefariki, ameumbika!

Huzuni iliyonipata ghafla si rahisi kuielezea lakini baada ya kurejewa na fahamu nilipata faraja kuwa chachage tutazidi kuwa naye katika maandishi ikiwemo kazi niliyokuwa naifuatlia kwake. Chachage alipumzika akiwa amemaliza kazi niliyotaka kuulizia. Simanzi hazijanisha nimeiona ripoti chachage aliyoituma siku chache kabla ya pumziko. Wangapi tutakamilisha kazi kabla ya kupumzika ?

Chachage amekuwa kijana muda wote. Ni mwezeshaji katika Semina za vijana na wanawake, kama alivyo mwasilisha mada Movenpick na Golden Tulip. Matamasha ya Jinsia, Chachage ni Mraghbishi. Uandishi wa vitabu vya Jinsia, yeye ni Mhariri. Utafiti wa kitaifa, nani kama yeye ? Kuhojiwa na Rioba, Makwaia na Ulimwengu, Chachage atachekesha! Lazima niseme wazi, Chachage ameumbika!

Ana marafiki wengi, vijana kwa wazee. Wanaume ni marafiki, kina mama na kina dada. Katika harakati zetu, Haijalishi ni wapi. Chachage tukiwa Zanzibar kweli alibunga bongo. Tulipokwenda Morogoro, jioni tulibarizi. Tukiwa na wakongwe wengine, Mwami, Shivji, Koda, Isinika, Kamata, Shamge, kwa uchache. Usiamini kwa nini, Chachage ameumbika ?

Safarini nilizipata, nasaha zake Chachage. Mumbai na Cape Town kwa shughuli tofauti. Maswali niliuliza, majibu sikuyapata. Chachage ni mchokozi hatoi jibu haraka. Katika watu makini, Chachage ndio mfano. Kwa kuwa msema ukweli, nani anamfikia ?

Buriani wetu Chachage, watu walisema sana. Yatosha kujisemea Chachage umeumbika. Changamoto iliyopo, tumebaki Chachage Wangapi?

**Deus M.Kibamba, Mwanafunzi na rafiki mkubwa wa Seithy L.Chachage katika mapambano dhidi ya mifumo kandamizi.**

## Twiga Katoroka, Kajiheshimu

Nimemkosa,
Sikumuona.
Akisimama wima,
Kama askari,
Na kiburi chake.

Kwa heshima na taadhima,
Akiimba kwa sauti nyororo:
"Mabibi na Mabwana,
Nawakaribisha kwenye
ndege hii ya Serengeti,
ndege ya Shirika la Ndege la Taifa."

Twiga ameruka,
Kenda kwao.
Kwao upo?
Mahali pake mkiani
Peupeeeee ....!
Nyeupe ya rangi,
rangi ya ubaguzi.

Ninashindwa,
kumeza.
Mkate na mayai, yao:
*Prepared and Packed*
*in Pretoria.*

Nimeinamisha kichwa.
Ninatetemeka kwa aibu.
Nawaona kwa kuibia,
Dada zangu wawili,
Wanyonge.
Bila tashi wala tamaa.

*"Here we're,*
*Carlesberg for you, sir."*
"na...na ... naomba safari."
*"Sorry... er..."*

Twiga katoroka,
Kenda na heshima zake.
(Kajiheshimu)
Katorokea wapi?
Mbuga zao,
Watalii wao,
Ndege yao.
Kibendera chetu!

*"**Jambo**!*
*Captain Roaming Rogue speaking."*

Buriani Twiga.
Kwaheri ya kuonana.
Kama sio kesho,
Keshokutwa.

***

**Issa Bin Mariamu**

KUMBUKIZI LA MWANAFUNZI

# CHACHAGE: Mwalimu Asiyechosha Kumsikiliza

Na Bernard Paul Baha



*Enzi tuishizo sasa ni enzi za kuonyeshana ubabe na pengine unyama waziwazi. Ni enzi za kutambiana kwa kutumia majina ya 'wazito' hata miongoni mwa walio wadogo kama sisimizi. Ulaghai na hata utapeli zimekuwa fani ambazo baadhi ya watu wamekubuhu. Na kwa njia hizo, mapenzi hulazimishwa na utajiri na madaraka hutafutwa kwa udi na uvumba. Chachage, C.S.L* ***Almasi za bandia*** *DUP 1987.*

Ni mwaka mmoja sasa tangu kamaradi huyu mahiri katika jamii yetu ajiunge na wahenga, lakini kwa baadhi yetu inakuwa kama tukio hili ni la jana. Binafsi kumbukumbu zangu bado ni makini kabisa kuhusiana na msomi huyu aliyeamua kulikana tabaka lake na kuamua kusema na kujitambulisha na mapambano ya wanyonge na wanafunzi katika maisha yake kama msomi na mwanamapinduzi. Bila shaka wanafunzi wote makini pale Mlimani watakubaliana na mimi kwamba huyu alikuwa ni tunu kwetu wote tuliobahatika kukutana naye pale Mlimani iwe katika mihadhara pale ukumbi wa Nkrumah ama hata katika *makorido* ya Mlimani. Sio kazi rahisi kutoa wasifu wa kamaradi Chachage ikizingatiwa kwamba alikuwa karibu katika kila sehemu, harakati za utetezi wa wanyonge, taaluma, muziki wa kizazi kipya na hata cha zamani, mshauri na mzazi, katika makala hii nitajaribu kupitia yale yote ninayoyakumbuka katika kipindi ambacho nilipata kuwa karibu ama kushuhudia mijadala aliyoshiriki kamaradi.

Binafsi nilimfahamu Profesa Chachage kwa mara ya kwanza kabisa baada ya kujiunga na Chuo kikuu cha Dar es Salaam mnamo mwaka wa 2003. Shauku yangu ya kujifunza na kuhudhuria mijadala ndiyo iliyonileta karibu naye. Katika kipindi chote nilichokuwepo hapo mlimani kamaradi hakuwahi kukosa katika mijadala mbalimbali ambayo ilikuwa ikiandaliwa na UDASA, ama DUPSA (Chama cha Wanafunzi wanaosoma Sayansi ya Siasa na utawala) ama Wanasoshiologia chini ya UDASUSO ama mijadala makini yoyote. Katika mijadala, kilichonivutia pamoja na mbwembwe zake katika kutengeneza maneno na kuweka mizaha ilikuwa ni jinsi alivyokuwa na uwezo wa kuwasilisha ujumbe kwa lugha nyepesi na akaeleweka. Hapa nazungumzia juu ya fikra za kimapinduzi za ukombozi wa wanyonge na sio nadharia za darasani ambazo kwanza wengi inakuwa ngumu kuzipata kirahisi hata pale anapotokea mhadhiri makini kwasababu ya ukosefu wa vitabu na uchache wake katika maktaba zetu.

Nimeamua kunukuu ujumbe hapo juu kutoka katika riwaya ya Almasi za bandia kuonyesha jinsi hadithi hiyo ya kusadikika ilivyoakisi mazingira ya Tanzania ya leo na kuonyesha hasa aina gani ya jamii tuliyokuwa nayo leo hii. Hata miongoni mwa wasomi ni wachache wanaotumia ujuzi wao kwa nia ya dhati ya kuleta mabadiliko ya kweli ya Mtanzania wa kawaida kutoka katika tabaka la walalahoi. Wakulima, Wafugaji na Wafanyakazi mara nyingi wanatumiwa katika miradi ya kujitajirisha ya wasomi wa leo. Lugha kubwa ikiwa ni ujasiriamali, ubinafsi ukiwa umeshika hatamu kila mmoja kati ya hawa ndugu waliobahatika kupata shahada ana tafuta mbinu mbalimbali ya kutengeneza mazingira ya kujinyakulia kilichobaki matokeo yake leo hii tuna makada na wanaojifanya ni makada na wapenzi wa chama tawala lengo ikiwa kujiandalia mazingira ya kupata madaraka yatakayowasaidia kujitajirisha zaidi.Waliobaki wapo katika asasi mbalimbali ambazo vikao na posho za safari ni wimbo wa kila leo, wengine wamejibanza kwenye vyama mbalimbali vya siasa wakiwa na matumaini ya siku moja wakikamata ikulu basi ni zamu yao kuchuma alimuradi kila mmoja ameamua kuwa ni mjasiriamali akitengeneza ama kuitumia mianya inayojitokeza. Maisha ya bandia ni kitu cha kawaida na hasa kundi la vijana kuficha uasilia na kujitanabahisha na tabaka tawala ni mambo ya kawaida. Haya yote hayakukwepa uchambuzi yakinifu wa Kamaradi Chachage kila alipopata nafasi ya kuongea, wapo waliopata kuitwa ni makuwadi wa soko huria, mabeberu waliobatizwa upya na kuitwa wadau wa maendeleo nao hawakuepuka mashambulizi ya kamaradi.

Mnamo mwaka 2004 hayati Chachage alijitokeza waziwazi na akapambana na VC (Makamu mkuu wa chuo wakati huo) jinsi alivyoshughulikia swala la kufukuzwa kwa Wanachuo waliogoma kupinga uanzishwaji wa bodi ya mikopo na vipengele mbalimbali katika mswada uliokuwa unasomwa bungeni.Wanafunzi wote tulitimuliwa jioni baada ya maandamano ya siku mbili na mapambano na FFU,wenzetu wengine walikamatwa. Inasemekana katika maandamano hayo kulikuwa na uporaji wa mali za watu katika eneo la Survey! Kwahiyo tulionyesha utovu wa nidhamu wa hali ya juu! Hayati Chachage wakati huo akiwa ni Mwenyekiti wa UDASA alitoa tamko la UDASA kupinga wanachuo kutimuliwa lakini pia na kukanusha juu ya wizi tuliozushiwa baada ya uchunguzi wa UDASA kubainisha kwamba hakuna kitu kama hicho kilichojitokeza. Mjadala uliofuatia baada ya hapo kati ya Kamaradi Chachage na Makamu Mkuu wa Chuo ulichangia kwa namna moja uharakishwaji wa kurejea kwetu Chuoni na pia tukapewa ruhusa ya kufanya maandamano ya amani mpaka viwanja vya Jangwani, nyimbo za kumsifia Chachage zilihanikiza maandamano hayo kuonyesha jinsi wote tulivyoukubali mchango wake.

Katika vitu vilivyokuwa vikimuudhi ni jinsi ambavyo tulikuwa tukiandaa mikutano yetu ya mijadala. Mara nyingi tulipendelea kuwaita viongozi wa vyama na serikali katika mijadala. Kuwapata hawa waheshimiwa ni kazi inayohitaji kuandika makala mpya! Urasimu uliopo haueleweki krahisi!. Siku zote kamaradi Chachage akituambia hakuna haja ya watu kama hao hasa wale wanaoitwa wageni rasmi. Siku moja nakumbuka hatuna mgeni rasmi na tulivyomwomba awe mgeni rasmi hakusita wala kutwambia tumwandalie hotuba ya ufunguzi alisisitiza hatuhitaji mgeni rasmi. Alipenda tuandae mambo yetu kwa umakini lakini tusiyafanye kuwa magumu kwa kutafuta wakubwa ambao kuwapata VC lazima ataarifiwe na apitishe juu ya kuja hawa waheshimiwa kwa jina la mgeni rasmi. Tunajohitaji alisisitiza siku zote ni watu wa kawaida, jumuiya ya wafanyakazi na wanafunzi na wakazi wa kawaida ama yeyote anayependa kushiriki katika mijadala.

Mijadala hiyo ilikuwa mara nyingi inaendelea mpaka nje, nakumbuka wakati fulani tuliandaa mjadala ambao ulihusisha viongozi wa nyama vya siasa ilikuwa ni kipindi cha karibu na Uchaguzi, ilikuwa taabu sana kuwapata viongozi wa CCM lakini baada ya kusikia ujio wa ndugu Mbowe aliyekuwa mgombea kwa tiketi ya CHADEMA, ndugu Philip Mangula wakati huo Katibu Mkuu wa Chama alifika kuwakilisha Chama pamoja na majukumu aliyokuwa nayo wakati huo na uzinduzi wa kampeni mikoani. Baada ya mjadala nilimdadisi ndugu Chachage juu ya vyama vyetu hivi na akanijibu kwamba hajaona mbadala, ilikuwa vigumu kumwelewa, kwamba pamoja na utitiri huu wa vyama bado tulikuwa hatujapata mbadala wa CCM na akasema si kwamba binafsi anakipigia chapuo CCM lakini misingi ya vyama vyote hivi kikiwemo CCM haikubeba udhati wa kumkomboa mnyonge na

Endelea uk. 11

Inatoka uk 10

# CHACHAGE: Mwalimu asiyechosha kumsikiliza

akanitania kwanini tusiunde chama mbadala na yeye yupo radhi kuwa mwanachama! Nilikuja kuelewa ni nini maana yake baadaye. Kimsingi ni kwamba kama wachambuzi wengine wa mifumo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi ya afrika, mfumo wa demokrasia wakilishi (Parliamentary democracy) una matatizo mengi na hauwakilishi hasa mawazo na matakwa ya walio wengi hasa ukiwa unatawaliwa na vyama vya siasa. Vyama mara nyingi hasa katika nchi kama Tanzania vinawasilisha maslahi yao zaidi. Nadhani hapa mifano tunayo mingi pale inapotokea kuna kusigana ama mgongano kati ya Serikali na bunge, rungu la chama hutumika kuzima upinzani wa wabunge hata kama matakwa ya wananchi yanahatarishwa.

Vikundi mbadala nje ya Chama ama vyama ni aina nzuri ya jinsi tunavyoweza kupata nguvu ya pamoja kufanikisha yale tunayoyoaona kama maslahi ya waliowengi. Lakini kuna ulazima wanachama wawe wameiva kisiasa na wanajua ni nini wanapaswa kufanya. Bahati mbaya Kamaradi aliondoka mapema kabla hatujafikia hatua ya kuanza kuandaa ni namna gani vikundi kama hivi vinapaswa viwe ama vianzishweje.

Mfumo mwingine uliopata upinzani kutoka kwa kamaradi ni NGOs akizipa majina aina aina,kama vile next government Officers, nothing is going on nk. Mkutano yao akiipamba kwa masihala nakumbuka safari moja akisema wanaitisha matukano ili wapate shitting allowance( matukano kwa maana ya mikutano) hii ni kwasababu ukweli ni kwamba nyingi za NGO zina malengo ya kuwatajirisha kama inavyoonesha nukuu hapo juu ni ulaghai wa hali ya juu wa kutumia shida za watu kutunisha mifuko ya wana NGOs, Kama tuna zaidi ya NGO na vikundi vya kiraia zaidi ya ishirini elfu ni kwanini hatujafika tunakotaka kwenda ama hata kuweza kubadilisha mtazamo na namna serikali inavyofanya kazi? Kwenye Mkutano mkuu wa HAKIARDHI uliofanyika Morogoro Kamaradi alizishambulia sana NGO akionyesha mapungufu yake na kutanabahisha dhahiri kwamba si vyombo vya mabadiliko hata kidogo. Alitoa wito kwa vyama vya wafanyakazi kuunda nguvu na baadhi ya taasisi makini za kiraia ili kutengeneza vuguvugu. Kwa njia ya vuguvugu walau ukombozi wa kweli unaweza kupatikana. Katika tamasha la Jinsia la mwaka 2005 linaloandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) kwa ushirikiano na FemAct, kamaradi hakusita kuwakosoa hawa wanaharakati kwa kutoweka mambo wazi, Kauli mbiu ya tamasha ilikuwa ni dunia bora na mbadala inawezekana, alihoji na kusema tunashindwa kitu gani kusema dunia mbadala ni ile ambayo hakuna unyonyaji na ubepari na jamii inaishi kwa misingi isiyotoa mwanya kwa tabaka moja kuja juu na kutawala jingine! (msisitizo ni wangu).

*Toleo hili maalum la Jarida la Ardhi ni Uhai ni tabaruku ya Marehemu Profesa Seith Loti Chachage aliyekuwa Mshirika wa karibu wa Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa Haki za Ardhi na mhimili wa harakati za utetezi wa haki za ardhi kwa wazalishaji wadogo wadogo.*

*Wanachama wa Hakiardhi, Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wote kwa pamoja tunaungana na umma wa wapenda haki wa Tanzania kukumbuka mwaka mmoja tangu shujaa huyu wa mapambano aage dunia hapo Julai 9, 2006.*

*Tunapenda kutoa rai kwa wapenda haki wote kumuenzi Marehemu Profesa Chachage kwa kuendeleza harakati za kumkomboa mwananchi mnyonge wa Tanzania kutoka katika mifumo kandamizi ya kibeberu pamoja na sera zake.*

*ALUTA KONTINUA*

Mchango wake ni mkubwa sana kwa fikra alizotuachia katika makala na vitabu vyake mbalimbali. Nimalizie kumbukizi hii kwa namna nilivyopokea taarifa za kifo cha kamaradi, kwanza kabisa nilikuwa ni mtafiti msaidizi katika kazi aliyokuwa anafanya na mhadhiri mwingine wa Idara ya Sayansi ya Siasa na Utawala ya Chuo kikuu Dar es Salaam, tulikuwa tunafanya tathmini ya Programu za HAKIARDHI katika wilaya za Kilosa na Hanang'. Baada ya safari ya Kilosa nilitakiwa kwenda Hanang' na Kamaradi Chachage, bahati mbaya akawa ana majukumu mengine ya kitaifa hivyo nikalazimika kuondoka na mtafiti mewingine tena, baada ya kazi ya siku kama tatu tulirejea na kukubaliana kukamilisha ripoti jumapili ya tarehe 9/7/2006. Ili tumkabidhi ripoti jumatatu ya tarehe 10. Asubuhi baada ya kufika kazini wakati tunaongea na baadhi ya wafanyakazi wenzangu mwenzetu ndugu Myenzi alipigiwa simu na kamaradi Kamata na baada ya hapo hakuna aliyeamini kilichotokea, ndugu Rasul naye alinitumia ujumbe kwa njia ya simu. Baada ya hapo kazi zilisimama ikabidi twende tukajumuike na wafiwa na ndugu wengine Changanyikeni wote tukijiuliza ni nini kimetokea.

Kamaradi amelala,tunaona wote ufa na pengo alililoliacha,bila shaka mchango wake ulikuwa bado unahitajika. Katika wakati huu ambao inaonekana wasemao ukweli wote ni watu waliopitwa na wakati wasiotaka mabadiliko na wasio ona mbali ni wachache wenye moyo kama wa Kamaradi ambao kama anavyosema katika Almasi za bandia yabidi mtu atawaliwe na moyo na sio kichwa. Mwili wenye kichwa kisichokuwa na moyo ni mzoga unaositahili kuliwa na fisi na tai. Akili hutetereka lakini upendo kwa watu haufi. Tunapofikiria mstakabali wetu leo kama wanyonge watanzania tuliodharauliwa na tunaoendelea kudharauliwa kama tusiokuwa na uwezo wa kufikiri,wavivu na wenye wivu kama wanavyosema watawala wetu, nadhani kunahaja ya kufanya kama anavyotushauri kamaradi Chachage na kwa kumalizia niwarudishe tena katika Almasi za bandia anapotuasa kwamba; Tufikiri yatokayo moyoni, sio yale yatokayo kichwani. Vitu huhisika moyoni, moyo hata siku moja haufi, lakini akili hutetereka ikatufisha hisia. Maisha maana yake halisi ni uzuri kupambana dhidi ya ubaya. Jamii si muungano wa watu bali uhusiano wao ndio uikamilishayo jamii. Na katika jamii iliyojaa ubinafsi kama hii, tushuhudiacho ni utokomezaji wa kila lililo jema kwa kisingizio cha kujenga wema.

Kwa habari na makala mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa USIKOSE Nakala yako ya Jarida la

ambalo hutolewa mara tatu kwa mwaka

**ARDHI NI UHAI**

HAKIARDHI ARDHI NI UHAI

# TUMKUMBUKE CHACHAGE KWA MANENO NA VITENDO

*Na. Ally Abbas Yusuph*

Kufa ni kitu kisichoepukika kwa njia yoyote, kwa mtu yeyote. Lau kungekuwa na aina yeyote ile ya kuwezesha baadhi ya watu wema wenye busara na hekima, basi jamii ingekuwa tayari kulipia gharama za kinga kwa wale watu wenye sifa stahiki na zilizo adimu ili wabaki kama hazina kwa jamii. Miongoni mwa watu hao kwa upande wangu au chaguo langu lingekuwa kwa Profesa Chachage Seithy L. Chachage na sio tu ningeomba abaki mzima, bali pia ili aendelee na jitihada zake za kuikumbusha jamii, iendelee na harakati za kujikomboa.

Marehemu Profesa Chachage alikuwa mwaharakati wa ukombozi wa jamii. Chachage alitumia elimu yake, nguvu na mali zake kwa makusidio ya ukombozi wa jamii yetu ya Tanzania. Marehemu Chachage mwenyewe alikuwa hapendi kujiita au kuitwa mwanaharakati, sababu zilizomfanya asipende kuitwa au kujiita hivyo alikuwa akisema kuwa "WANAHARAKATI SIO WA KWELI" kwa hiyo Marehemu Chachage alipenda aitwe MUJAHIDINA. Kwa sababu mujahidina ndio wa kweli; "MIE SIO MWAHARAKATI, MIE MUJAHIDINA. WANAHARAKATI SIO WATU WA KWELI" Maneno haya aliyatamka tarehe 26.11.2004 kwenye mazungumzo yaliyoandaliwa na shirika la HAKIARDHI juu ya nafasi ya Vyama vya Kiraia katika Mfumo wa Kisasa yaliyofanyika Zanzibar tarehe 26-27.11.2004.

Kauli hii ya kujitamba kuwa hataki kuitwa mwana harakati bali aitwe mujahidina kwangu ilizidisha kumuona kuwa mtu anayejitolea maisha yake kwa ajili ya watu wenzake.

Nilimuhesabu kwa sifa hii kutokana na maana halisi ya neno lenyewe "MUJAHIDI" kwa hiyo mujahidina ni watu wanaofanya kazi za kujikomboa wao wenyewe pamoja na jamii kwa jumla. Kazi ya kujikomboa au ukombozi, mkombozi anahitaji awe na zana za kuendeshea shughuli za ukombozi. Moja miongoni mwa zana za kuendeshea shughuli za ukombozi ni elimu, zana ambayo marehemu alikuwa miongoni mwa wa Tanzania wachache waliobahatika kuipata na ambao waliweza kuitumia kwa kuendeleza ukombozi wa Taifa letu.

Marehemu Profesa Chachage alikamilika kwa kila eneo kwani kuwa mtu kamili si kazi ndogo. Ukiachilia mbali, sifa za kimaumbile, sifa moja zaidi ya kimaumbile ni elimu, ushauri na kukubali kukosolewa. Haya yote alikuwa nayo marehemu Chachage kwa hiyo kufa kwake sio msiba tu, bali ni pengo kubwa kwa Mujahidina kama mwenyewe alivyokuwa akipenda kuitwa. Ni sawa kuwa ametutoka kwavile tusingeweza kuzuia japo tulimpenda, lakini sisi ambao bado tungali hai tunayo nafasi kubwa ya kushirikiana nae kwa kuenzi na kuendeleza harakati za ukombozi kwa kutumia maarifa yake ambayo ametuachia. Mwanafalsafa mmoja kwa zama zake alisema kuwa ***'Hafi machoni isipokuwa haonekani'*** kwa kuamini fikira hii basi Profesa Chachage hakufa bali tumetenganishwa nae, bado kimawazo tunae; kama ilivyokuwa kwake mwenyewe hakuwasahau kamwe wanaharakati waliopambana na watawala wa kijeremani, VITA VYA MAJIMAJI, wanaharakati hao ilikuwa ndio marejeo yake kwenye maandishi yake. Nao ni akina Bwana Heri, Machemba, Mkwawa Sapi, Kinjekitile na wengineo, nasi kwetu itakuwa ni marejeo yetu kwake.

Nimesema huko nyuma kuwa Profesa Chachage alikuwa miongoni mwa wasomi wachache waliotumia elimu zao kwa faida ya kuwanusuru waliowengi ambao wanadhulumiwa na wasomi walio wengi ambao wamesomeshwa na jasho la wanaowadhulumu. Kwan nchi za kiafrika, wasomi hao wakiwemo Marais, Mawaziri, Wabunge na Mahakimu ndio walio msitari wa mbele kukandamiza wananchi waliowapa dhamana ya kuwaongoza. Badala ya kuwa chachu ya maendeleo kwa jamii, taasisi zao ndizo hugeuka kuwa vyanzo vya maonevu kwa jamii. Kwa mfano, serikali inapotayarisha mswada wenye lengo la kuwadhulumu wanyonge, Bunge likaupitisha, mahakama wakaukubali na Rais akaidhinisha kuwa sheria kisha watendaji wa serikali wakatekeleza kwa madai wanatekeleza kazi kwa mujibu wa sheria. Bila kujali sheria hiyo inaathiri jamii vipi na kwa kiasi gani. Hawa ndio wasomi wa kundi la kwanza ambao husimama kw[a] nia ya kuja kufanya manyanyaso kwa jamii zetu. Hawa ndio Marehemu profesa Chachage pengine aliamua kukataa kuitwa mwana HARAKATI kwaajili yao.

Marehemu Profesa Chachage nimemtaja kuwa alikuwa mtu anayeshaurika. Binafsi nimelishuhudia hili pale nilipo shauri kuwa *paper* zinazoletwa kwenye semina na makongamano ni nzuri lakini ujumbe wake haufiki kwa walengwa kwakuwa huamdikwa katika lugha wasiyoijua. Haya niliyasema kwenye Mkutano Mkuu wa Wanachama wa HAKIARDHI siku ya tarehe 26.11.2004 Zanzibar. Marehemu Profesa Chachage alipata somo maridhawa kutokana na ushauri huo na mara alianza kuandika makala aliyoiita "MAPAMBANO YA UMMA DHIDI YA MBINU ZA KINYANYASAJI NA UKANDAMIZAJI" kwa Kiswahili fasaha. Majumuisho ya makala hizo ndiyo yaliyounda mada nzito kwenye Kongamano la Kitaifa juu ya Haki za Ardhi za Wazalishaji Wadogo Wadogo tarehe 12-13/05/2005 kwenye ukumbi wa Baraza la Maaskofu Kurasini, Dar es Salaam.

Makala hizi ziliwafanya wahusika kufahamu juhudi zinazofanywa na wasomi wachache ambao wana nia ya kuleta mabadiliko ya sera katika jamii. Basi miongoni mwetu kama kweli tunamkumbuka Profesa Chachage hususani wanaharakati wa haki za Ardhi, utawala Bora, Haki za Binaadam basi tumkumbuke kwa maneno na vitendo.

**Anuani/Ofisi**
Taasisi ya Utafiti na utetezi wa Haki za Ardhi **(HAKIARDHI)**, Sinza Mori
S.L.P. 75885, DSM, Tanzania. Simu: +255 22 2771360 /Faksi: +255 22 2771362, +255 784 646 752.
E-mail: info@hakiardhi.org Tovuti: www.hakiardhi.org